



REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI
THIRD ASSEMBLY-THIRD SESSION

THE HANSARD

Wednesday, 24th April 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 2:30 p.m.*

[The Deputy Speaker (Hon. Kombo) in the Chair]

PRAYER

STATEMENT

DISTRIBUTION OF LOCKERS TO VOCATIONAL TRAINING CENTERS

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Members, there is a Response to a Statement that was raised earlier but I ruled that the Response be taken back to the House Business Committee for reallocation of time. Next order!

(Statement deferred)

MOTION

ROAD GRADERS FOR EACH SUB-COUNTY

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. I beg to move the following Motion:

THAT, aware that public roads improve access to social amenities such as schools, hospitals and markets which in turn boost the living standards through creation of employment opportunities and promotion of trade within the County and the Country at large.

FURTHER AWARE THAT, in the Kilifi County Integrated Development Plan that is (CIPD) of 2023-2027, the objective of the transportation strategy that includes connecting production areas to potential markets and upgrading existing road networks to enhance accessibility.

NOTING WITH CONCERN THAT, Kilifi County residents have for many years been grappling with transportation challenges due to poor impassable roads especially during rainy sessions.

This County Assembly, therefore, urges the County Executive Committee Member (CECM) in charge of the Department of Transport and Public Works to ensure each of the Seven Sub-Counties has a functional road grader for efficient and timely construction and maintenance of the roads.

I wish to submit my contributions before I call upon the seconder. We are from a rainy season, and we are still on it, and we are all aware from our various wards that our roads are impassable due to the heavy rains that we experience in our last season.

Mr. Speaker, I am aware that that county only had two graders that were not functioning, they were grounded and this morning, I want to take this opportunity to applaud the Governor His excellency Gideon Maitha Mung'aro for commissioning two new graders. Again, that gives us a total number of four of which the two as still grounded therefore, Mr. Speaker, we need at least seven. If the economy of this County allows, which is in my prayer and my wish that the economy expands so that we have a grader in each ward.

Mr. Speaker, there has been a problem with our roads. Personally, from my ward, I have experienced a lot of difficulties in terms of impassable roads. Recently, when there was distribution of examination papers, some schools were not accessible because of the impassable roads. I personally remember employing men to at least repair some roads so that the exams can reach certain schools.

There have also been challenges with ambulances; they do not even at the moment reach some areas so as to carry and assist patients to hospital. For the economy to grow, they must reach the relevant markets for sales and sustainability of our family. There are donors and investors who normally do favors in schools and institutions; for example, the other time in Kimbule Primary School, we had a donor who was building classes, halls and toilets in one institution they wanted to upgrade the institution but the road to deliver materials to the schools was a nightmare. With the community, we came together and did handy jobs to make sure the road was repaired for the lorry transporting the material to access the construction area.

With those few remarks, it is evident that we need these graders so that there can be a rationale of the graders from one ward to the other within the Sub-Counties. We have seven Sub-Counties, example in Ganze Sub-County, we have four wards namely Ganze, Bamba represented by Hon. Mohamed, Jaribuni by Hon. Shehe we have Sokoke by Hon. Thaura so if we have just one grader that is functional, there can be a rationale of the grader for one ward to the other as we wait for the improvement of this County so that we can have a grader in each ward.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

It is reasonable that we need these graders. At the moment, we have four and only two are functioning. I have spoken to the *Waziri*, they are doing their level best to repair them and be functional but again, we need an additional five new ones so that every sub-county can have a new grader. This can be done in the next financial year through the Committee on Transport led by hon. Mkadi; we make sure there is allocation of about five new graders and meet our mission of a grader in each Sub-County. I urge Members of this House to support the Motion so that we can have sustainable development in the county. With that, let me call the seconder hon. Tete to second.

Hon. Tete: Asante, mhehsimiwa Spika. Naunga mkono Hoja iliyozungumziwa na mheshimiwa wa Ganze Benson Ngirani. Asante.

(Question proposed)

Hon. Kubo: Asante sana, kwa nafasi hii. Nasimama kuunga mkono Hoja hii nikijua kwamba barabara ni kitu cha maana sana haswa katika Kilifi Kaunti yote. Nikiongea haswa kuhusu wadi yangu, barabara nyingi hazipitiki na hizi barabara zinapotengenezwa huwa hazina *maintainance* kwa sababu ya upungufu wa hizi *graders*. Naamini kwamba tukiweza kupata *grader* hizo na kila *sub-county* kweli nafikiria tutaweza kutunza barabara zetu na tuweze pia kudumisha maendeleo ya Kilifi *County* kwa jumla. Namshukuru pia mheshimiwa Ngirani kwa Hoja hiyo. Asante.

Hon. Kea: Asante sana, Bw. Spika. Pia mimi nataka kuungana na wenzangu kuunga mkono Hoja hii ya hizi tingatinga za kulima barabara. Nataka pia kumshukurun mheshimiwa wa Ganze, Bw. Benson Karisa Ngirani Maneno kwa kuona mbali mambo haya ya barabara. Bw. Ngirani ni jirani yangu sehemu zile za Kibarani, tumepakana upande ule wa juu.

Shida ya barabara imekua donda sugu kwa Kilifi Kaunti yetu ambapo sasa inabidi sote kama waheshimiwa tuungane mkono na jambo kama hili tuone kwamba kila *sub-county* inapata tingatinga lake na barabara zetu ziweza kutengezwa. Magari yamekua mengi sasa lakini yanaharibika kila uchao na hata pesa za kuzitengeza hakuna. Leo ilitibi ni je ya tuk tuk kwa sababu ya hali mbaya za barabara, kile kigari changu kiliharibika.

Nasikitika kwa sababu mimi kama mheshimiwa naweza kujikakamua na nikatengeza gari lakini yule mwananchi ambaye mapato yake ni duni anapata shida kila uchao katika kuendeleza taifa hili la Kenya. Sasa wakati wa mvua umeanza na unaendelea ni kwamba usafiri utakua shida sana na hata watu wengine kufika kwa kazi itakua tatizo. Hivi juzi kulikua na mvua kubwa sana, ilikua ni *mini* el nino na watu walikua na matunda yao angalau waweze kupeleka sokoni lakini ikashindikana na mazao mengi yaliozea shambani wa watu hawakuweza kupata fedha kutokana na mazao yao.

Ombi langu ni kwamba, yule mkuu wa kitengo cha usafiri katika Kaunti yetu ya Kilifi atufanyie mpango. Leo zile tinga tinga mbili ambazo zimeanzishwa na mtstahiki Gavana zitasaidia mahali pakubwa lakini ingekua vizuri sana; Kilifi *North* yenyewe iko na wadi saba ambazo sasa tinga tinga moja peke yake haitoshi lakini kwa sababu ya kugawanya hapa na pale kwa muda hiyo pia itatusaidia pakubwa sana.

Ninao ufahamu kwamba hali za uchumi katika nchi yetu ya Kenya ni mgumu lakini pia watakapotuongezea haya matinga tinga yatakua yametusaidia pakubwa ili tuweze kujikimu katika mahitaji yetu ya kila siku, barabara lazima ziwe zinapitika. Hili si ombi kwa *County Executive* peke yake lakini nataka kuomba hata serikali ya kitaifa; barabara yetu ya kutoka

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Ganze-Bamba mpaka kufikia Kilifi ilikwamia hapo katikati na imefanya sehemu hiyo haipitiki kabisa. Ni ombi langu kwamba hili litatiliwa maanani, litazingatiwa kwa ukamilifu na watu wa Kilifi wakapate kusaidika. Naunga mkono. Asante.

Hon. Thuara: Asante, mheshimiwa Spika. Kwanza ningeomba nimpongeze ndugu yangu ambaye pia ni jirani yangu mheshimiwa Benson Karisa Ngirani kwa kuleta Hoja hii. Katika *submissions* zake kama alivyotangulia, amezitaja faida za barabara na sote kama wajumbe tunazifahamu na pia wananchi wanazifahamu kwamba inakua rahisi kama barabara ziko hali nzuri kufanya shughuli zetu za kawaida.

Mfano, mheshimiwa Spika, katika wadi ambayo natoka, asilimia 99 ya barabara zimeharibika kulingana na hali ya mvua. Naona kisiasa kidogo tunakosa sura na sijui labda, mheshimiwa Spika, utakua na utofauti kule unakotoka lakini unaweza ukafanya miradi mingi sana lakini barabara ni kitu ambacho kila mtu anakiona kwa hivyo sisi kama wajumbe; kwa sababu nafikiri wengi ama sote hapa bado tuko na ari ya kuendelea kuwa kwenye siasa basi moja kwa moja nafikiri hiyo itakua ni njia moja ya kutukwamua katika hasira za wanachi kwa sababu sasa hivi wananchi wana hasira kwa ajili ya barabara zilivyo.

Naunga mkono kwamba kama ndugu yangu Karisa Ngirani alivyosema, tunahitaji hata kama ni hiyo *sub-county* tuwe nainga tanga moja lakini ninachoomba zaidi ni kwamba najua inawezekana kwa sababu bajeti tuko nazo, ni sisi tunaopanga tupange kulingana na *priority*. Ikiwezekana tupange kwa kila wadi iwe nainga tanga lake na itakua ni njia mojawapo ya kupatia vijana ajira kwa sababu kama itakua niinga tanga 35 ina maana kuna vijana 35 ambao watakua wamepata ajira. Kwa hivyo, mimi hiyo naiunga mkono asilimia mia na kusema kwamba hilo ikiwezekana kwa uharaka zaidi, mheshimiwa Spika.

Hon. Paul: Asante sana, mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nataka nimuunge mkono mheshimiwa Ngirani kwa kuleta Hoja hii ambayo kwa kweli imekua tatizo sana. Mimi ni mjumbe wa Magarini *Ward* ambayo kwa jina kuu limesimamia Magarini *Sub-County*. Kwa kweli barabara zetu ziko hali mbaya. Naunga mkono kwa dhati hili jambo ya kwamba kupatikaneinga tanga ambazo zitawezesha kulimwa zile barabara zote ziwe zitakuwa katika hali nzuri. Amegusia kwamba, kuna zile barabara ambazo wakati mwingi wagonjwa huwa wanahitaji kubebwa na kupelekwa kwa rufaa. Kusema ukweli, ni kwamba mimi tayari nimeathirika mwaka jana wakati ule mvua kali ya *el nino*. Mama alikua anataka kujifunguwa ikabidi abebwe na kitanda asafirishwe ili aweze kupata usafiri wa kuelekea hospitali.

Ni hali ngumu lakini hili jambo tulichukulie sisi kama waheshimiwa la maana sana na wale ambao wanakalia hii Bajeti waliangalie kwa kina sana ili zile barabara zote ambazo zimeharibika zirekebishike wale vijana wetu ambao wanatubeba na pikipiki wawe wanaweza kuwasafirisha wananchi wetu kwa njia nzuri, kwa hivyo, ninaunga mkono. Saa hii ninavyoongea, kuna barabara zingine zimefekwa na maji. Mto Galana umefurika na maji na barabara zingine saa hii hazipitiki. Lakini ikiwa itafikia wakati kwamba hizi barabara zikitengenezwa vizuri hata zile sehemu maji yameleta shida hizo pia nina hakika zitarekebishika na wananchi watakua na wakati mzuri wa kutembea kwa njia nzuri.

Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, nataka niunge mkono mia kwa mia na mheshimiwa Ngirani uendelee hivyo hivyo, Ganze itakukumbuka. Asante.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Paul. Mheshimiwa Brown Safari.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Brown: Asante sana, Bw. Spika, ninafurahia sana kuunga mkono Hoja hii maana ni Hoja ambayo ina manufaaniliyokuwa nikiiombea Maulana aipitishie na iweze kuhakikishwa kwamba itaangaziwa.

Mheshimiwa Spika, mimi najua wenzangu wamezungumza kuhusu maswala ya barabara huwa ni mbaya kwa sababu ya msimu wa mvua. Kitu mimi ningependa kuangazia kwa saa hii ni sehemu ya kwangu kule Mtepeni. Mabwenyenye hawana nafasi za kujenga nyumba zao, zile nafasi za barabara siku hizi zimekua ndio sehemu za wao kutengeneza titles na kujenga. Kwa hivyo, ikiwa hizi tingatinga zitapatikana kuna barabara zengine ambazo zinatajikana zifunguliwe na ziwe zitakua na urahisi watu wawe na upenyo wa kupitisha mali zao na kufanya shughuli zao za kawaida.

Kwa hivyo, mimi napongeza sana ndugu yangu Karisa kwa kuangazia Jambo hili na nina amini sisi wajumbe sote katika Jimbo letu tukufu la hapa Kilifi tutaliunga mkono na tutilie mkazo katika Bajeti ili tumuunge mkono Gavana wetu na tuunge mkono sera hii kuonyesha kwamba barabara zitaweza kutayarishwa wakati wowote. Ijapokuwa Gavana kwa *manifesto* yake ni kwamba anahitaji kuona kwamba lami zitaingia katika kila pande ya nyanja zetu, lakini huu ni mwanzo mpya ambao naupongeza nikiamini kwamba Bunge letu liko macho na kuhakikisha kwamba tunaunga mkono katika sera zetu pamoja na sera za Gavana. Nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Asanteni.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante sana, mheshimiwa Brown Safari. Wacha tusikie kwa mheshimiwa Grace Wambui.

Hon. Grace: Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia fursa hii. Nimesimama kuunga mkono huu Mjadala na kumshukuru sana mheshimiwa Ngirani kwa kuuleta kwa sababu katika kila mji kuendelea lazima barabara ziwe ziko sawa. Mimi nikiwa hapa nimeletwa kama mwakilishi wa wanawake kwa kizungu *gender top up*. Ningelisema kuwa katika maendeleo, wamama huteseka sana na kuteseka ni kwa sababu barabara hakuna. Kwa mfano, mimi nimezunguka katika hii Kaunti na nimepata kuna mahali hata barabara hazipitiki na barabara zikiwa zimetengenezwa na zinapitika biashara zinafunguka, ajira zinapatikana na hapo ndio unapata wamama hawateseki kwa sababu kutakuwa na ajira, kutakuwa na maendeleo, kutakuwa na masoko. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru mheshimiwa Ngirani kwa kuja na hilo wazo na kuuliza Idara husika iweze kuharakisha ili barabra zetu ziweze kufunguka angalau maendeleo yaweze kumfikia mwananchi. Asante, Bw. Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante sana, mheshimiwa Grace. Wacha tusikie kutoka kwa mheshimiwa Ibrahim.

The Leader of Majority (Hon. Ibrahim): Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Ningetaka kusimama hapa kuunga mkono Hoja ambao imeletwa na mheshimiwa Ngirani. Ni jambo la muhimu na pia ninampongeza kwa kuuleta Hoja hii kwa sababu ameona kuna matatizo na kuna uhitaji ndio maana akakaa akafikiria ndio akaleta Hoja hii na umuhimu wa sisi kama waheshimiwa kuletwa katika Bunge hili ni kwamba tunaangalia yale matatizo ambayo yana kumba wananchi wetu ili tuweze kuuleta Hoja kama hii. Itakuwa si vyema leo mheshimiwa umalize miaka mitano hapa ndani ya Bunge hii bila kuuleta Hoja yoyote wa kusaidia wananchi wako wa Jimbo letu la Kilifi.

Nataka kumpongeza mheshimiwa Ngirani kwa kuuleta Hoja hii. Ni Hoja ambayo itanufaisha wananchi wetu, ni Hoja ambayo italeta maendeleo kwa wananchi wetu. Mambo ya barabara yatafunguka na kitu muhimu ni kwamba kazi ya mheshimiwa Ngirani ameshaitimiza, sisi kama Wabunge tumeshaitimiza kazi zetu. Kitu muhimu sasa, Bw. Spika, ni kwa Mwenyekiti

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

wa Kamati ya Barabara awe anayafutilia mambo kama haya. Tukumbuke kwamba tunapo kadiria Bajeti, kila wizara ina harakisha kuweka miradi yao na Mwenyekiti wa Bajeti huwa hana mamlaka ya kusema kwamba kuna Hoja ililetwa kwamba magari ya kusafisha barabara yanunuliwe kwa kila *sub-county*. Huwa hana mamlaka yale, mamlaka yale ni Mwenyekiti akae na Waziri na *Chief Officer*, Idara yao asukume kwamba mimi kama Mwenyekiti kuna Hoja ililetwa na mheshimiwa Ngirani na Hoja ile ikapitishwa Bunge kwa hivyo, ningepomba Waziri hii iletwe ipelekwa kwa Kamati ya Bajeti na ipitishwe haya magari yawekwe kwenye bajeti na hapo ndio itakua kila mtu ametimiza majukumu yake. Kwa sababu si vyema leo Hoja kama hii imeletwa hapa kisha Mwenyekiti asishughulikie aseme wao watatengeza. Kunatakikana msukumo kwa sababu wizara ni nyingi na kila wizara inatetea mambo yake.

Na ukiona alieleta Hoja hii; mheshimiwa Ngirani amesema kwamba leo hii Gavana amezindua tinga tinga mbili za kusafisha barabara, ni kwamba Gavana mwenyewe pia hamu yake pia ata furahikia akiona kwamba tumemsaidia kupitisha Hoja ya kuzidi kununua magari kama yale. Kwa hivyo, kitu muhimu ni kila mtu awe na majukumu yake, jukumu la Ngirani ameshaleta jukumu la Bunge hili ameshapitisha sasa ni jukumu ya Mwenyekiti kusukuma kwenda kukaa na Kamati yake ya Bunge hili kuhakikisha makatibu wa Kamati yake wamepeleka stakabadhi ambazo zimepitishwa hapa na yeye awe anafuatilia. Asante sana, Bw. Spika. Kwa haya machache, nataka kumshukuru mheshimiwa Ngirani.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante sana, mheshimiwa Ibrahim kwa changizo zako za kihakikama. Wacha tusikie kutoka kwa mheshimiwa Said Kadhengi (Mohamed).

Hon. Mohamed: Shukuran, Bw. Spika, kwa kuweza kunipatia furasa hii. Pia, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupatia uhai hadi kufikia hapa. Mimi pia, niungane na wenzangu kuunga mkono Hoja hii na pia kuweza kumshukuru mheshimiwa Ngirani kwa sababu Hoja hii wazungu husema “*was long overdue*” maanake kiuweli ni kwamba barabara zetu ziko hali mbaya na tumejaribu sana ila ni kama alivyo tujua mheshimiwa Ngirani kwamba Idara ilikuwa na matingatiga mawili ambayo yalikuwa hayafanyi kazi vyema.

Hali za barabara zetu nikipeana mfano wa Bamba ni mbaya sana. Kiukweli nikiungana na mheshimiwa Grace aliyesema kwamba wamama wanateseka, kule Bamba wamama wanateseka na si kwa kuwa labda ni mambo ya lishe wala nini, ila ni kwa sababu ya hali ya usafiri wa kutoka sehemu mmoja hadi nyengine. Wamama wakiwa waja wazito tumeweza kushuhudia wakizaa njiani kwa sababu hali ya barabara ni mbaya; kuna mama alibebwa kwa bodaboda na kwa hali ya ubaya wa barabara ile basi mama huyu wa Kilifi ikabidi azae njiani.

Mimi nafikiri jukumu ambalo limebaki sasa kama wenzangu vile unavyo ona mheshimiwa Spika, Bunge iko tayari kupitisha Hoja hii. Hoja itakuwa imepita, sasa ombi langu kama Kiongozi wa Wengi alivyosema ni kwamba sasa msukumo utabaki kwa Idara. Tunajua tumebaki na siku kidogo ambapo hali ya Bajeti inaenda kutekelezwa hivyo basi ingekuwa vyema kama Idara itachukulia na uzito ule ambao Bunge hii imechukulia Hoja hii na kuweza kutenga kiasi cha fedha ambacho kitawezesha ununuzi wa tinga tinga hizi ili baada ya musimu huu wa mvua ambao sasa tutaingia, pengine Mwezi wa Saba ambapo kutakuwa na kiangazi, basi tingatinga hizi kama zitakuwa zimepatikana zitakuwa za msaada kwa sababu zitafanya kazi na barabara zetu zitaweza kurekebisha. Mimi naungana na wenzangu kuunga mkono Hoja hii. Asante.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Said (Mohamed). Wacha tusikie kwa mheshimiwa Mary Anzazi (Maneno).

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Maneno: Asante, Bw. Spika, kwa kunipatia fursa hii. Nami pia nimesimama kuunga mkono Hoja ambayo iko mbele yetu ya kuongeza tingatinga ili ziweze kuenda kwa maeneo Bunge saba yetu ya Kilifi.

Bwana Spika, Hoja hii imekuja kwa wakati mwafaka. Barabara zetu zikiwa sawa hata uchumi wa Gatuzi yetu ya Kilifi utapanda, ushuru utapatikana na huduma zitafanyika bila wasiwasi. Ninabaki kuunga mkono Hoja hii na kumpongeza, kumpa kongole mheshimiwa Ngirani wa Ganze. Ndugu yangu, wewe naona umekuwa wa manufaa kwa Bunge hili kwa sababu Hoja kama hii si ya Ganze pekee bali kwa Gatuzi lote la Kilifi. Asante sana, pia kwa Mstahiki Gavana, kwa leo ameweza kuzindua yale tinga tinga mawili na naamini baada ya bajeti tukiwekewa hata kama ni tinga tinga mawili, mwaka mwengine tena wa kifedha tuwekewe mawili, Bw. Spika, baada ya miaka mitano tutakuwa tumepiga hatua kubwa. Ninaunga mkono. Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Asante, mheshimiwa Mary (Maneno). Mheshimiwa Stephen Baya wakati ni wako.

Hon. Stephen: Asante sana, Bw. Spika, kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, nataka kushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuleta katika Bunge hili ili kwamba tuweze kutetea wale watu wetu ambao walituchagua.

Pili, ningependa kumushukuru mheshimiwa Ngirani kwa kuleta Hoja hii hapa Bungeni ambayo ni Hoja muhimu sana. Mimi nawakilisha watu wa Wadi ya Gongoni na kama kuna shida ya barabara basi ile Wadi yangu ina shida ya barabara sana. Ijapo tunajaribu, lakini zile shida bado ziko. Nitapeana mfano wa barabara ya kutoka Mjanaheri kuenda Ngomeni; hiyo barabara ni yangu mimi na mheshimiwa Paul wa Magarini. Hiyo barabara ndiyo inayopitisha yale malori makubwa ambayo yanachukua mchanga kupeleka Mombasa.

Mchanga wote ambao unapeleka Mombasa, Kilifi na Kaunti yote na nje ya Kaunti unatoka kule kwangu Ngomeni. Kusema kweli, ile barabara ni mbaya na imekuwa ikisumbua magari kwa muda mrefu sana. Kuna wakati nilimpeleka Waziri na *Chief Officer* kuona hiyo barabara lakini wakasema matinga tinga ya kulima kwa Kaunti yetu yalikuwa hayako. Sasa Hoja hii ikipita na tuwe na tinga tinga moja Magarini, itakuwa mahali popote barabara itakuwa imeleta shida basi ni kuongea tu na dereva wa tinga tinga na mahali hapo paweze kutengenezwa mara moja. Barabara yangu ya kutoka Povuni hadi Shomela imemea manyasi mpaka hiyo barabara ya kupitia magari imebaki kidogo sana ambapo kama tungekuwa na tinga tinga moja hapa Magarini hiyo barabara ingeenda kulimwa angalau ikapanuliwa magari yakapita vizuri na wananchi wangepurahi sana.

Waheshimiwa wenzangu, barabara zikiwa mbaya sisi hutukanwa sana hususan kama tumetoka nyumbani tunakuja kazini. Tunasemekana hapa Bungeni tumelala, hatufanyi kazi lakini naamini Hoja hii itakapita na matinga tinga yakinunuliwa, shida hizi za barabara hata kama hazitaisha lakini zitapungua. Mimi naunga mkono na ningependa Hoja hii tupitiche na najua utapita. Ninachoomba ni kuwa Hoja hii ichukuliwe ni wa maana sana hata kama yale mengine yatasimama lakini mimi ningependa kwa Bajeti hii inakuja tuwekewe pesa ili kwamba tuweze kununua haya matinga tinga. Nashukuru pia Mstahiki Gavana, leo pia ameanzisha yale matinga tinga mawili lakini yakiongezewa, basi barabara zetu zitakuwa sawa.

Nimesimama hapa kuunga mkono na mheshimiwa Ngirani, Mungu akubariki na ningependa waheshimiwa wote hapa ikifika wakati wa kuuliza lile swali sisi sote tupitiche mara moja na yale mengine yaje baadaye. Kwa hayo machache ama mengi, nasema Mungu awabariki.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Mheshimiwa Philister Meso.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Meso: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this chance. Hon.Ngirani congratulations on this wonderful Motion.

Mr. Speaker, the way I see the mood of the House, why can't you just put the Question and then we clear everything because none of us has gone against it? Everybody is supporting it, so just put the Question. Thank you, so much Mr. Speaker, Sir.

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Thank you, Hon. (Ms.) Meso; let us hear from Hon.Tete before we conclude the Motion.

Hon.Tete: Asante tena kwa mara ya pili, Bw. Spika. Ninapenda kuanza kwa kusema kuzaa si kazi, kazi ni kumulea mwana. Naizungumza hii misemo ya wahenga kwa sababu hizi *graders* hazinunuliwi kwa mara ya kwanza kwa Kaunti yetu ya Kilifi, zimekuweco na kupitia kwa muzungumzaji wa kwanza ambaye amepeana hii *Motion*, alikuwa wazi akasema ziko ambazo hazifanyi kazi na ninakumbuka kipindi kifupi kilichopita nimesikia kuwa kulikuwa na *grader* sehemu za Magarini ambayo ilikaa huko muda mpaka ikakatwa katwa na kuuzwa *scrap* na ilikuwa mali ya Kaunti. Hiyo ilikuwa pesa ya umma ambayo siku moja ilikaliwa na mtu mwenye maono kama hivi Bunge likapitisha chombo kile kikanunuliwa kikawa ni kiwe faida kwa wana Kilifi na leo hii kiliuzwa *scrap*.

Maono na malengo ni mazuri lakini utekelezaji; hizi *graders* ambazo tunazitungumzia hazitafanya kazi, zitafanyiwa kazi na ikiwa tutasifu kwamba hivi vyombo vikija katika barabara zetu zitang'ara haziwezi kung'arisha ni mipangilio ndio itakayo ng'arisha. Nasimama nikisema kwamba maono ya Gavana, mapenzi ya Bunge hili ni kuona Kilifi Kaunti yetu inafanyiwa kazi katika hali za kisawa sawa.

Hivi juzi, wakulima walioko ndani ya Kilifi Kaunti walilalamika tinga tinga hazitoshi, ni kidogo na zilikosa mafuta. Kunao wahesimiwa hapa niliwasikia wakisema ya kwamba wamepigiwa simu na wakaazi wa maeneo yao wakisema wameambiwa waeke mafuta tinga tinga wakalimiwe halafu gharama hizo watakatwa juu kwa juu. Hizi tinga tinga ni zetu sisi kama Kaunti, halafu zinatushinda ku *maintain* mpaka mwananchi wanaambiwa wakatafute pesa za kulimiwa *acre* zile wanataka wapatie dereva wakawawekee mafuta walimiwe zitakazobaki watafanyiwa mahesabu. Kuzaa, sio kazi ni kulea.

Nasimama kwa mara nyingine kusema tunataka Mawaziri wenye kupanga kazi na kushirikiana na Kamati husika ili mambo kama haya yasipiatikane. Kwa mfano, kama Kamati ya Kilimo na Bajeti watu wawe wabunifu kiasi cha kujua kwamba hivi vyombo havikuletwa vikae. Kule kwangu shimo la Tewa tuna *schemes* ambazo zinakatwa mpaka leo na zikiisha kukatwa lazima kutolewa barabara, vyombo kama hivi ndio vinatakikana Wizara ziwe zinaweza kushurutisha viende mashinani kubuni barabara lakini mpaka saa hii hakuna barabara ambazo zimepasuliwa kwa sababu hakuna hivi vyombo.

Kila wakati tunaambiwa chombo kiko lakini hakuna mafuta, sasa tunanunua vya kazi gani wakati Waziri hawezi kujipanga na kitu kama hicho. Nasimama na kusema sisi kama Bunge tunapitisha Hoja hii na mawaziri ni wale wale tulio waleta hapa wakati tunaonyesha wana Kilifi kwamba tuna nia njema nao, tunahitaji kuona wamesimama watekeleze zile nia ndio kesho wananchi wetu watakuwa na imani na sisi.

Hivi vyombo havijanunuliwa kutupa sifa tu, zina gharama fulani ambazo zikisimamiwa vizuri serikali yetu itakuwa imepunguza mzigo mkubwa wa matumizi. Mfano, saa hii *light grading* zina gharimu shilingi milioni tatu; hiyo ni pesa ya mwananchi inaenda na hakuna kitu kimetengenezwa na kufinika mchanga tu kutoka mahali pamoja hadi kwingine.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hizi zinasaidia kupunguza gharama kama hizo na ile pesa ikasimama kununuliwa saruji, kama kutakuwa hakuna mipangilio mizuri, tinga tinga zitakuwa na tutakuja kumbuka kwamba iko siku tulizungumza haya na yametimia na kutimia kwake ni kwamba zilizo oza hata hizi pia huenda zikaoza. Hongera, mheshimiwa Ngirani, kwa mtazamo huu wa kutupea Hoja hii tuizungumzie. Ni maono mazuri tunayaunga mkono na Gavana maono yake yalikuwa haya kwamba tutapunguza gharama katika Kaunti kwa kununua vyombo vya kufanyia ukarabati barabara zetu na hicho ni chanzo lakini walioko pale tunataka waige mfano wa Gavana. Je, ni nini anataka? na tuweze kutekeleza.

Asante, kwa hii nafasi. Sikujua kama niki *second* bado naweza kuongea, ndio maana nime *second* halafu nikangoja wakati wangu. Asante.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. I want to take this opportunity to appreciate the House and honourable Members in support of this Motion. This Motion will see five new graders and we urge the CECM in charge of Roads to repair the two old graders and have stand-by graders from the two that were officiated today by His Excellency the Governor. We urge the next budget to have five new graders so that we have seven new graders and the two old ones to be repaired and be stand-by graders in case there is a breakdown of the new ones.

I urge the Implementation Committee to do the due diligence and follow up with the relevant Department that is Roads to make sure that there is 100% implementation of this Motion with the assistance of the Roads Committee to make sure budgetary allocations for this financial year 2024/2025 is implemented with a view of this Motion. I also want to echo what hon. Tete has just said, that in coming up with these graders we will be saving a lot of money from the taxpayer.

We are moving slowly; maybe in the next budget, we will have another Motion that we have at least two tippers of murrum in every ward or even one in every ward so that we do away with the tendering system of maintenance of roads. This year alone during the submission of the budget ceiling, there is about Kshs230 million allocated for road maintenance and as the Member has put it, is just a matter of doing a shoddy job and someone is going home with a lot of money.

With this, we will do away with road tendering on maintenance so that we can save the taxpayers money. It is also a way of strengthening the implementation of the Governor's manifesto so that we see good roads and uplifting the face of Kilifi roads.

With those remarks, Mr. Speaker, I again thank my fellow honourable Members. Thank you.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

The Deputy Speaker (Hon. Kombo): Hon. Members, we have come to the end of this session, and we adjourn until Monday at 2.30 p.m.

The House rose at 3:23 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*